

## **Kairuki: Jamii nzima ishiriki kutatua matatizo ya Maadili.**

Serikali imesema jamii nzima inatakiwa kushirikiana kutatua matatizo ya mmomonyoko wa maadili unaolikabili Taifa badala ya kuacha tatizo hili kushughulikiwa na vyombo vya dola pekee.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Angellah Kairuki katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Bi. Suzan Mlawi jijini Dar es Salaam wakati akifungua Mdahalo wa wadau kuhusu Kujenga na Kukuza Maadili, Haki za Binadamu, Uwajibikaji na Utawala Bora na Mapambano dhidi ya Rushwa.

Alisema, “suala la maadili sio jukumu la Rais, vyama vya siasa, vyombo vya dola au taasisi simamizi za utawala bora, bali ni suala la jamii mzima.”

“Kadri siku zinavyokwenda, suala la maadili linazidi kuwa changamoto, sio Tanzania tu bali dunia nzima. Mfano mauaji ya albino na mambo mengine, vyombo vya dola pekee haviwezi kulitatua, lazima jamii nzima ishiriki katika kulitatua,” alisema.

Kwa upande wake Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais Mstaafu Jaji Joseph Warioba alisema, “tatizo la maadili huwezi kulitafutia dawa ya haraka, wala huwezi kutengeneza maadili katika jamii kwa kutunga sheria, lazima kuwepo na misingi itakayohakikisha maadili yanalindwa na kusimamiwa.”

Akichangia mada katika mdahalo huo, Jaji Warioba alieleza kuwa, lazima kuwe na miiko ya uongozi na kuwepo na taasisi za kusimamia miiko hiyo ili kurejesha maadili nchini.

Kiongozi huyo Mstaafu alifafanua kuwa kama serikali inataka kurejesha maadili, iipe uwezo Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ili zifanye kazi bila kuingiliwa kisiasa kama ilivyo Ofisi ya Mkaguzi na Mdhhibiti wa Hesabu za Serikali (CAG). “Ukiimarisha vyombo hivi, vikawa na nguvu ukawa pia na misingi ya uongozi maadili yatarejea.”

Naye Kamishna wa Maadili Jaji (Mst) Salome Kaganda alisema ugonjwa wa baadhi ya viongozi kuvuka mipaka ya mamlaka yao katika mihimili ya dola unachangia kwa kiasi kikubwa uvunjifu wa maadili nchini.

“Kuna ugonjwa wa watu kuvuka mipaka ya mamlaka ya kazi zao, tunapochanganya majukumu tunasababisha udhaifu mkubwa kimaadili. Tuheshimu utawala wa sheria na kuzingatia mipaka ya kazi zetu ili kuepuka uvunjifu wa maadili,” alisema.

Mdahalo huo ni sehemu ya Maadhimisho ya Siku ya Maadili yanayoandaliwa na kuratibiwa na taasisi zinazohusika na masuala ya utawala bora nchini ambapo kilele chake itakuwa Desemba 10, 2016 katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam.

Taasisi hizo ni Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Tasisi ya Kuzuia na kupambana na Rushwa, Mamlaka ya Kudhibiti Manunuzi ya Umma, na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali.

Taasisi nyingine ni Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Tume ya Utumishi wa Umma na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.